TANGAZO LA SERIKALI NA. 873 la tarehe 1/12/2023

SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI,
(SURA YA 148)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 6)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI KATIKA MRADI WA UANZISHWAJI WA KILIMO CHA MIWA NA KIWANDA CHA KUZALISHA SUKARI CHA KAMPUNI YA M/S MUFINDI PAPER MILLS LIMITED YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika mradi wa uanzishwaji wa kilimo cha miwa na kiwanda cha kuzalisha sukari cha kampuni ya M/S Mufindi Paper Mills Limited ya Mwaka 2023, na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 22 Septemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, msamaha unatolewa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani inayopaswa kulipwa kwa bidhaa na huduma zilizoainishwa katika Jedwali la Amri hii zilizoingizwa nchini au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na au kwa niaba ya Kampuni ya M/S Mufindi Paper Mills Limited kwa ajili ya uanzishwaji wa kilimo cha miwa na kiwanda cha kuzalisha sukari.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na Kodi ya Ongezeko la Thamani itapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa bidhaa zitatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 22 Septemba, 2024 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya M/S Mufindi Paper Mills Limited na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BIDHAA

| NA. | MAELEZO | KIPIMO | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Truck with concrete mixer | Nos | 10 |
| 2. | Truck with concrete pump | Nos | 5 |
| 3. | Ambulance 4WD | Nos | 2 |
| 4. | Ambulance 4WD | Nos | 2 |
| 5. | Low bed Trailers | Nos | 10 |
| 6. | Rigid trucks | Nos | 100 |
| 7. | Box body truck | Nos | 80 |
| 8. | Water bowsers | Nos | 60 |
| 9. | Diesel Bowsers | Nos | 40 |
| 10. | Trailer Covered | Nos | 140 |
| 11. | Trailer Flatbed/Tankers | Nos | 100 |
| 12. | Water Tankers | Nos | 100 |
| 13. | Bucket and Ripper Tines | Nos | 15 |
| 14. | KG Dozer Blades and Tree Pusher Bar | Nos | 100 |
| 15. | 4X4 Single Cabin Pick ups | Nos | 150 |
| 16. | Tippers | Nos | 200 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17. | Horse Tractor | Nos | 300 |
| 18. | Mini Bus | Nos | 30 |
| 19. | Bus | Nos | 20 |
| 20. | Hard tops | Nos | 100 |
| 21. | 4x4 Double Cabin Pick UPS | Nos | 150 |
| 22. | Motor Cycles-Farm Security OPS | Nos | 1200 |
| 23. | Executive Mini Bus | Nos | 10 |
| 24. | Single Cab Toyota Land Cruiser Pickup | Nos | 40 |
| 25. | Boat with Engines | Nos | 20 |
| 26. | Forklift | Nos | 30 |
| 27. | Mobile Crane | | 30 |
| 28. | Tractor tyres | | 20,000 |
| 29. | Truck Tyres | | 30,000 |
| 30. | Trailer Tyres | | 30,000 |
| 31. | Lathe and Workshop Machinery | | 1,000 |
| 32. | Diesel | Litres | 12,000,000 |
| 33. | Engine Oil | Litres | 300,000 |

Dodoma,
21 Novemba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*